# HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 07/10/2021 KILICHOFANYIKA KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA.

### MAHUDHURIO YA WAJUMBE

### WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Elizabeth M. Gumbo | Mkurugenzi Mtendaji (W) | M/Kiti |
| 2. | Bw. Michael Tolage | Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi (W) | Katibu |
| 3. | Bw. Filbert Kanyilizu | Katibu Tawala (W) | Mjumbe |
| 4. | Bw. Sile Salmini | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara (W) | Mjumbe |
| 5. | Mwl. Mtobi K. Edward | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari (W) | Mjumbe |
| 6. | Bw. Kita Charles | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango na Takwimu (W) | Mjumbe |
| 7. | Bw. Joshua S. Shayo | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria (W) | Mjumbe |
| 8. | Bw. Harauna Taratibu | Afisa Habari (W) | Mjumbe |
| 9. | Bw. Robert O. Kibongolo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira (W) | Mjumbe |
| 10. | Bw. Jonathan J. Buluba | Mratibu wa Kamati ya Kudhibiti UKIMWI (W) | Mjumbe |
| 11. | Bw. Mateso P. Kaswanu | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji (W) | Mjumbe |
| 12. | Bw. Josiah Msiba | Afisa Biashara (W) | Mjumbe |
| 13. | Bw. Joshua Kelly | Kny.Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (W) | Mjumbe |
| 14. | Bw. Hagai Usiri | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki (W) | Mjumbe |
| 15. | Bw. Msese K. Msese | Mwenyekiti wa Timu ya Mapato (W) | Mjumbe |
| 16. | Bi. Happiness M. Komba | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi (W) | Mjumbe |
| 17. | Bi. Ester Msigala | Kny.Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii (W) | Mjumbe |
| 18. | Eng. Mussa Ezekile | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi (W) | Mjumbe |
| 19. | Bw. Mwishauri M. Matuki | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA (W) | Mjumbe |
| 20. | Bw. Ngandu Jacob | Kny. Mkuu wa Idara ya Afya (W) | Mjumbe |
| 21. | Mwl. John Mpamwa | Kny. Mkuu wa Idara ya Msingi (W) | Mjumbe |
| 22. | Bw. Malula M. Gogadi | Karani wa Kamati za Kudumu/Kaimu A/Uchaguzi | |

### WAJUMBE WASIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Dr. Kiraba Msoke | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi | Kwa taarifa |
| 2. | Bw. Stephen Simba | Mkuu wa Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule | Kwa taarifa |
| 3. | Bw. Julius D. Sayi | Katibu wa TSC | Kwa taarifa |

### MUHT.CMT NA 01/04/10/2021: KUFUNGUA KIKAO

Katibu wa kikao aliwajulisha wajumbe kuwa kwa mujibu wa kitabu cha Mahudhurio akidi ya wajumbe ilikuwa imetimia. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao. Mwenyekiti



Scanned with CamScanner

alifungua kikao saa 04:05 asubuhi kwa kuwataka wajumbe kujadili kwa makini agenda zilizoandaliwa.

**MUHT.CMT NA 02/04/10/2021: KUTHIBITISHA AGENDA.**

Katibu wa Kikao aliwasilisha agenda za kikao kama ifuatavyo:

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 10/9/2021
4. Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha tarehe 10/9/2021
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi mwezi Septemba, 2021
6. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Julai-Septemba, 2021
7. Maombi ya Kubadili Matumizi ya Fedha za Jengo la Utawala Tsh.400,000,000/=
8. Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi Julai-Septemba, 2021
9. Taarifa ya Ununuzi wa gari moja aina ya 'TOYOTA L/CRUISER HARD TOP 5DOOR MANUAL'
10. Taarifa ya Majibu ya Hoja za Ukaguzi wa Ndani zilizosalia robo ya IV,2020/2021
11. Taarifa ya Taratibu za Uanzishwaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo (Township Authority)
12. Taarifa ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Mabaraza ya Kata
13. Taarifa ya uanzishwaji wa Anwani za Mitaa
14. Taarifa ya mapokezi ya Hati za Usajili wa Vijiji 102
15. Taarifa ya Tathimini ya Ujenzi wa Uzio wa Minada ya Laini na Migato
16. Taarifa ya Kutengewa fedha za kujenga Majosho mawili ya kuogesha mifugo kiasi cha Tsh.36,000,000.00
17. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha za Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO – 19 Tsh.2,450,000,000.00
18. Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Serikali Kiidara Julai-Septemba, 2021
19. Taarifa ya Utekelezaji wa maazimio ya kikao cha Kmati ya Fedha, Utawala na Mipango tarehe 17/09/2021
20. Kuahirisha kikao

Wajumbe waliunga mkono agenda hizo zijadiliwe kama zilivyoandaliwa.

**MUHT.CMT NA 03/04/10/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 10/09/2021.**

Muhtasari ulisomwa mbele ya wajumbe, Muhtasari ulipokelewa na haukuwa na marekebisho. Kisha wajumbe waliunga mkono kuwa muhtasari ni sahihi, hivyo ulitiwa saini na kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao cha tarehe 10/09/2021.

**MUHT.CMT NA 04/04/10/2021: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 10/09/2021.**
**Azimio Na.1: Mwenyekiti wa Kikosi Kazi cha Ukusanyaji Mapato awasilishe taarifa ya mapungufu ya gari lililokuwa likitumika kwenye shughuli za ukusanyaji mapato SM 3674 na gharama zinazohitajika za kulifanyia matengenezo gari hilo.**

Ilielezwa kuwa azimio lilitekelezwa. Gari SM.3674 lilikuwa na tatizo la matairi na rejeta. Taratibu za manunuzi na matengezezo ya gari hilo zinaendelea kufanyika. Wajumbe



Scanned with CamScanner

waaliagiza taarifa ya matengenezo ya gari hilo iwasilishwe kwenye kikao cha tarehe 11/10/2021.

**Azimio Na.2: Taarifa ya Utengenezaji wa Vitambulisho vya Misamaha ya Wazee iwasilishwe katika kikao cha Morning prayer tarehe 13/9/2021**

Ilielezwa kuwa azimio lilitekelezwa, taarifa ya vitambulisho vya misamaha ya wazee iliwasilishwa katika kikao cha Morning prayer tarehe 13 Septemba, 2021.

**Azimio Na.3: Wakuu wa Idara na Vitengo walio na hoja za Ukaguzi wahakikishe wanajibu hoja zao na vielelezo kuwasilishwa kwa Mkaguzi wa Ndani kwa uhakiki.**

Ilielezwa kuwa azimio lilitekelezwa kwa baadhi ya Wakuu wa Idara. Hoja zilizosailia zinawahusu Idara ya Fedha , Idara ya Afya na Maendeleo ya Jamii.

**MUH.CMT NA 05/04/10/2021: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI MWEZI SEPTEMBA, 2021.**

Mweka Hazina wa Halmashauri kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Septemba, 2021 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ifuatavyo:

**MAPATO**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ina vyanzo vya mapato kama ifuatavyo;

**VYANZO VYA MAPATO YA NDANI**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima mwaka 2021/2022 ilikisia kukusanya jumla ya Tsh **1,307,035,716.00** kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ya ndani kwa mwaka 2021/2022. Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imekusanya kiasi cha **Tsh. 122,609,574.21** na hivyo kufanya mapato yote ya ndani katika kipindi cha julai,2021 hadi septemba, 2021 kuwa jumla ya **Tsh. 366,404,784.66** ambayo ni sawa na asilimia **28** ya makisio ya mapato ya ndani kwa mwaka 2021/2022.

**MAPATO YA FEDHA ZA MATUMIZI MENGINEYO ( OC) NA MISHAHARA**

Ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilikadiria kupokea fedha za ruzuku ya matumizi mengineyo, ruzuku ya vyanzo vilivyofutwa na ruzuku ya mishahara ya watumishi kiasi cha ***Tsh 19,632,513,459.00.*** Katika kipindi cha mwezi *Septemba*, 2021 Halmashauri imepokea fedha ya Ruzuku ya Matumizi Mengineyo ( OC) na Ruzuku ya Mishahara ya watumishi (PE) jumla ya Tsh **1,624,644,649.00** kwa mchanganuo ufuatavyo:

| NA | Maelezo | Makisio 2021/2022 | Pokelewa Julai- Agosti 2020/2021 | Pokelewa Septemba, 2021 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ruzuku ya matumizi mengineyo ( OC) | 1,526,830,001 | 30,709,999 | 185,212,499 | 14 |
| 2. | Ruzuku ya Mishahara( | 17,887,041,459 | 2,853,737,300 | 1,1,439,432,45 | 24 |



Scanned with CamScanner

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | PE) | | | 0 | |
| 3. | **JUMLA** | **19,413,871,459** | **1,602,076,899** | **1,624,644,950** | **23** |

**MAPATO YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO**

Ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ilikadiria kupokea fedha za ruzuku ya miradi ya maendeleo kiasi cha ***Tsh 11,818,159,629.00.*** Katika kipindi cha mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imepokea fedha **Tsh.115,749,210.00** kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo:

| NA | Maelezo | Maksio | Pokelewa Julai- Agosti, 2021 | Pokelewa Septemba, 2021 | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Elimu Bure - Msingi | 933,693,000 | 136,782,741 | 68,391,371 | 21 |
| 2 | Elimu Bure - Sekondari | 624,387,500 | 74,715,679 | 37,357,839 | 20 |
| 3 | Ukamilishaji wa Zahanati | 150,000,000 | 0.00 | 50,000,000 | 33 |
| | **JUMLA** | **1,708,080,500** | **211,498,420** | **155,749,210** | **21** |

**MATUMIZI**

Ilielezwa kuwa katika kipindi cha mwezi Septemba, 2021 Halmashauri imetumia jumla ya **Tsh 1,601,646,650.00** kwa ajili ya kugharamia Miradi mbalimbali ya maendeleo, kulipa mishahara ya watumishi na kugharamia shughuli mbalimbali za uendeshaji wa Halmashauri. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizi ni kama ifuatavyo:

- Matumizi ya Miradi ya Maendeleo — Tsh 105,749,210.00
- Matumizi Mishahara ya watumishi — Tsh 1,439,432,150.00
- Matumizi Mapato ya ndani — Tsh 6,672,000.00
- Matumizi ruzuku ya Matumizi Mengineyo — Tsh 155,542,500.00

**Jumla** — **Tsh 1,601,646,650.00**

Hivyo jumla ya matumizi yote ya Halmashauri katika kipindi cha mwezi Septemba 2021 ni **Tsh 5,082,585,301** sawa na **15%** ya makisio ya mwaka ya **Tsh 33,890,970,715.00.**

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa.

Kuhusu suala la ushuru wa mkonge, ilielezwa kuwa hivi sasa wanalipia ushuru kwa nusu tani kiasi cha Tsh.7,500/= kwa kuwa wanunuzi wanasafirisha kwa bajaji. Hivyo ICTO aingize kifungu cha ushuru wa mkonge nusu tani ili ushuru uweze kulipika kwenye POS. Aidha wajumbe walisisitiza mkonge usisafirishwe bila kibali.



Scanned with CamScanner

Kuhusu madeni ya ushuru wa pamba, kikao kilimtaka Afisa Kilimo awasilishe orodha ya Makampuni yaliyonunua pamba wilayani ambayo bado yanadaiwa ushuru na kikao kilisisitiza Sheria ndogo za Mapato zitumike kudhibiti ukusanyaji wa Mapato.

Kuhusu wakusanya mapato walio chini ya malengo, kikao kilimtaka Mweka Hazina afuatilie kwa kila mmoja kujua kiasi kilichokusanywa na kwa wale ambao hawakufikia malengo watakiwe kutoa maelezo sababu ya kutokusanya mapato kama ilivyopitishwa kwenye malengo ya kila Kata.

Kuhusu changamoto ya kutumika risiti moja kusafirisha mazao zaidi ya mara moja, kikao kilishauri watendaji wa Kata waelekezwe kusimamia usafirishaji wa mazao kwa wafanya biashara na kuhakikisha kuwa vibali vya kusafirishia mazao vinagongwa muhuri kwa tarehe husika ya kusafirisha mazao, vinginevyo tofauti na tarehe iliyoruhusiwa kusafirisha mazao mhusika atakuwa anahesabika kukiuka taratibu na hatua zichukuliwe.

Kuhusu hoja ya ununuzi wa Jenereta kwa ajili ya huduma ya nishati ya umeme katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya, taratibu za manunuzi zinaendelea kufanyika ambapo hatua za manunuzi zimefanyika. Vilevile kuhusu ujenzi wa uzio na kibanda cha walinzi, ilielezwa kuwa zabuni zitatangazwa hivi karibuni.

Aidha kikao kilimtaka Afisa Mipango kuhakikisha kuwa miradi yote ya ujenzi iliyoletewa fedha mwezi Juni, 2021 juhudi zifanyike ili ifikapo tarehe 30 Novemba, 2021 miradi hiyo iwe imekamilika na kukabidhiwa.

## MUHT.CMT NA 06/04/10/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO JULAI-SEPTEMBA, 2021

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya wilaya ya Itilima katika Bajeti ya mwaka 2021/2022 ilitenga kiasi cha **Tsh. 12,049,227,402.58** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya maendeleo. Aidha hadi kufikia Septemba, 2021 kiasi cha **Tsh. 1,720,072,106.81** za Miradi zilisalia kwenye akaunti ya maendeleo kama Bakaa ya mwaka 2020/2021.

### 1.1 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA ZA BAKAA 2020/2021.

Ilielezwa kuwa Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ilibaki na fedha kiasi cha **Tsh. 1,720,072,106.81** kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo kutoka katika vyanzo mbalimbali .

Aidha hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2021, Jumla ya Tsh. **411,549,924.48** zilikuwa zimetumika kukamilisha miradi hiyo na kubakia salio la Tsh **1,308,522,182.33** ambayo itaendelea kutekelezwa katika kipindi cha Robo ya II kwa mwaka wa fedha 2021/2022, mchanganuo wa matumizi ulikuwa umeambatanishwa.

### 1.2 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/2022

Ilielezwa kuwa Katika Bajeti ya Mwaka 2021/2022, Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha **Tsh.12,049,227,402.58** katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo,Kiasi hiki cha



Scanned with CamScanner

fedha kinatokana na Mapato ya ndani, Ruzuku kutoka Serikali kuu na Mifuko mbalimbali ya Wahisani.

Ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2021 jumla ya fedha kiasi cha **Tsh. 554,745,260.00** zimepokelewa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2020 jumla ya **Tsh. 554,745,260.00** zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kubaki na salio la **Tsh. 427,921,660.00,** mchanganuo wa matumizi ulikuwa umeambatanishwa.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuijadili.

Kuhusu ujenzi wa kituo cha Afya Kanadi, wajumbe walisisitiza wasimamizi waelekezwe kuzingatia viwango vya vifaa vinavyokusanywa na jamii kama vile kokoto, mawe na mchanga. Wananchi wahamasishwe kushiriki nguvu kazi na gharama zitafsiriwe.

Kuhusu ujenzi wa Bweni katika shule ya Msingi Lagangabilili, kikao kimesisitiza uhamasishaji kwa wananchi kusomba mchanga ufanyike kwani imeonekana kuwepo na mwitikio mdogo kwa wananchi kushiriki katika ujenzi huo.

Kuhusu fedha za mapato ya Ndani za mchango wa 40% kwenye miradi ya maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa kiasi cha Tsh.70 milioni, kikao kiliagiza kufikia tarehe 11/10/2021 ziwe zimeanza kutumika kwenye shule zilizopewa, vinginevyo vihamishiwe kwenye maeneo mengine.

Wajumbe walimtaka Afisa Mipango kurekebisha taarifa ya miradi ya maendeleo ili ioneshe uhalisia na hatua iliyofikiwa hadi siku ya kikao.

**MUHT.CMT NA 07/04/10/2021: MAOMBI YA KUBADILI MATUMIZI YA FEDHA ZA JENGO LA UTAWALA TSH.400,000,000/=**

Maombi ya kubadilisha matumizi ya fedha shilingi 400,000,000.00 ambazo zimetengwa katika Bajeti ya 2021/2022 kwa ajiii ya ujenzi wa Jengo la Utawala ambapo fedha kiasi cha shilingi 750,000,000.00 zilizotolewa mwaka wa fedha 2020/2021 zitakamilisha kazi zote zilizopangwa kwenye jengo la utawala.

Kutokana na hali hiyo nawasilisha ombi la kubadili matumizi ya fedha shilingi 400,000,000 .00 za ujenzi wa jengo la Utawala na kufanya kazi zifuatazo;

i. Ununuzi wa pikipiki 22 kwa watendaji wa kata shilingi 50,000,000.00
ii. Ukamilishaji wa zahanati 03 shilingi 150,000,000.00
iii. Ujenzi wa Nyumba za watumishi 03 shilingi 150,000,000.00
iv. Ujenzi wa nyumba 01 ya mtumishi hospitali ya Wilaya shilingi 50,000,000.00.

Wajumbe walihoji kuhusu maafisa ugani kuwa na usafiri. Ilielezwa kuwa kuna mpango wa bodi ya pamba kununua pikipiki kwa kila afisa ugani. Hivyo wakaunga mkono swala la usafiri kwa watendaji wa kata.

Kuhusu ujenzi wa nyumba za watumishi, wajumbe waliridhia maombi ya kubadilisha matumizi ya fedha kuwa yapite kama ilivyopendekezwa.

**MUHT.CMT. NA. 08/04/10/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MANUNUZI JULAI-SEPTEMBA, 2021**



Scanned with CamScanner

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima katika kipindi cha Robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 imetekeleza manunuzi yenye thamani ya **Tsh 98,027,323.00.** Wajumbe walipokea taarifa na kuijadili Katika majadiliano ilishauliwa kuwa manunuzi yaendelee kufanyika kwa kuzingatia sheria na taratibu za manunuzi.

**MUHT.CMT. NA. 09/04/10/2021: TAARIFA YA UNUNUZI WA GARI MOJA AINA YA 'TOYOTA L/CRUISER HARD TOP 5DOOR MANUAL'**

Ilielezwa kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha TZS 154,868,816.06 kwa ajili ya ununuzi wa "TOYOTA L/CRUISER HARD TOP 5DOOR MANUAL". Mchakato wa ununzi wa gari hilo ulikamilika ambapo tuliwalipa wakala wa ununuzi Serikalini (GPSA) kama sheria ya Ununuzi inavyotutaka.
Mnamo tarehe 05/10/2021 tulipokea barua kutoka kwa wakala wa Ununuzi Serikarini (GPSA) ya tarehe 12/08/2021 yenye kumbu Na. CDA.260/318/06/AW/151 iliyotujulisha kwamba kutakuwa na ucheleweshaji wa upatikanaji wa gari tulilolipia kutokana na uhaba wa vifaa vya TEHAMA duniani vinavyotumika katika utengenezaji wa magari. Hali hii inategemewa kuimarika ifikapo mwezi Januari 2022
Wakala wa Ununuzi ameahidi kutujulisha mara moja hitaji letu litakapowasili nchini kwa hatua za usajili na makabidhiano.
Wajumbe waliunga mkono na kuafiki wakashauri taratibu za manunuzi kuzingatiwa.

**MUHT.CMT. NA. 10/04/10/2021: TAARIFA YA MAJIBU YA HOJA ZA UKAGUZI WA NDANI ZILIZOSALIA APRILI - JUNI, 2021**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha robo ya nne, 2020/2021, jumla ya hoja 14 ziliibuliwa. Hoja 7 zilijibiwa na kufungwa na kubaki hoja 7 vinavyohitaji vielelezo na baadhi kusubiri kufanyika kwa vikao vya Bodi ya Zabuni. Vilevile bado kuna hoja za nyuma 12 ambazo hazijafungwa.

Wajumbe walipitia kila hoja na majibu yaliyotolewa. Katika majadiliano, kikao kiliagiza wahusika wote watafute majibu na kupeleka vielelezo kwa Mkaguzi wa Ndani ili vihakikiwe na hoja zifungwe.

**MUHT.CMT. NA. 11/04/10/2021: TAARIFA YA TARATIBU ZA UANZISHWAJI WA MAMLAKA YA MJI MDOGO (TOWNSHIP AUTHORITY)**

Ilielezwa kuwa Uanzishwaji wa Mamlaka za Miji Midogo unasimamiwa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sheria Namba 7 ya mwaka 1982. Sheria tajwa imeainisha kuwa mwenye mamlaka ya kuanzisha Mji Mdogo ni Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwenye maeneo yanayofaa au yanayopendekezwa kwa minajili ya kuimarisha ustawi, kuchochea maendeleo na usimamizi wa mifumo ya serikali za Mitaa.

Mamlaka ya Mji Mdogo baada ya kutangazwa huwa Mamlaka iliyohuishwa kisheria (body corporate) inayoweza kumiliki mali inayohamishika na isiyohamishika, inaweza pia kushtaki au kushtakiwa.

Mamlaka pendekezwa ya Mji Mdogo wa Luguru itaundwa na Kata moja (1) ya Luguru ambayo inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 18,328 kati yao wanawake ni 8,786 na



Scanned with CamScanner

wanaume 9,559 kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 Kata ya Luguru ina jumla ya Vijiji Vinne (4) na Vitongoji Ishirini na Tisa (29) .

Ilielezwa kuwa kabla ya utekelezaji elimu lazima itolewe kwa wananchi na wananchi wakiridhia mchakato unafuatwa. Wajumbe walihoji ni nani wenye wajibu wa kutoa elimu . Ilielezwa kuwa kamati ikilidhia Mkurugenzi atateua wataalamu wa kwenda kutoa elimu.

Wajumbe baada ya majadiliano kikao kilishauri gharama za uanzishaji mamlaka ya mji mdogo ziainishwe ili kuweza kuona kama Halmashauri itamudu kugharamia kuendesha halmashauri mbili na shughuli za uchaguzi kwa kuwa Halmashauri haina mapato ya kutosha.

**MUHT.CMT. NA. 12/04/10/2021: TAARIFA YA MWONGOZO WA UENDESHAJI WA MABARAZA YA KATA**

Mabaraza ya Kata na mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yamepewa mamlaka ya kutatua migogoro Mabaraza ya Kata na mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yamepewa mamlaka ya kutatua migogoro ya ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019 chini ya kifungu cha 167 (l), na kifungu cha 62 (2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura ya 114 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019, pia kifungu cha 3 cha Sheria ya Mabaraza ya Kata Sura ya 206, ambapo kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Mahakama za Ardhi (utatuzi wa migogoro) Sura ya 216 kimefanya Baraza la Kata kuwa Mahakama ya Ardhi ambayo itakuwa na jukumu la kusikiliza migogoro ya Ardhi kama ilivyokuwa Mahakama za mwanzo.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kupitia Kitengo cha Sheria ina jukumu la kusimamia uundwaji, uhuishwaji, kuyajengea uwezo na utekelezaji wa majukumu ya Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji yaliyopo katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.

Hivyo, tunaleta kwenu mapendekezo ya mwongozo wa viwango vya ada za Mabaraza ya Kata na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji unaokusudiwa kutumika katika Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ili viweze kujadiliwa na kupata ridhaa ya Halmashauri.

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuweka viwango vya ada vinavyolingana kwa Mabaraza yote ndani ya Halmashauri kama ilivyo Ada za Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya na Mahakama zingine.

Aidha kesi zote za jinai zitafunguliwa bila malipo isipokuwa mtuhumiwa akipatikana na hatia atatozwa faini kwa mujibu wa Sheria na Miongozo ya Mabaraza ya Kata.

Mapato yatakayopatikana yatatumika kama ifuatavyo;

20% - Posho ya Mwenyekiti

15% - Posho ya Katibu

15% - Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza mfano Ununuzi wa shajala, meza na viti.

40% - Posho ya Wajumbe

10% - Itapelekwa kwenye Kata kwa ajili ya usimamizi wa Mabaraza.



Scanned with CamScanner

Mapato kutokana na chanzo hiki yatakusanywa kupitia ofisi ya Mtendaji wa Kata na kutolewa stakabadhi halali. Baraza la Kata litarejeshewa 90% ya fedha walizokusanya na taarifa ya mapato na matumizi kusomwa katika vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) kila robo.Aidha, tarehe rasmi ya kuanza kutumika kwa Mwongozo huu itabainishwa baada ya kupata ridhaa ya vikao vya kisheria vya Halmashauri.

Wajumbe walishauri kianzishwe chanzo cha mapato ya ada ya mabaraza ya Kata na fedha zitakazokusanywa zibaki kwenye Mabaraza ya Kata na kutenga asilimia ya usimamizi kutoka Ofisi ya Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya.

**MUHT.CMT. NA. 13/04/10/2021: TAARIFA YA UANZISHWAJI WA ANWANI ZA MITAA**

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima inakusudia kuanzisha Mfumo wa Anwani za Makazi na Postkodi ambapo itahusisha majina ya barabara , njia, nambari katika nyumba za makazi na sehemu za biashara. Utekelezaji wa zoezi hili utarahisisha shughuli za mawasiliano pamoja na kupunguza vitendo vya uharifu nchini.

. Aidha, kutokana na ukuaji wa kasi wa maeneo na kutokuwepo kwa majina ya barabara, njia na nambari za nyumba umeleta changamoto katika utoaji wa huduma za kijamii, kiuchumi na uwekaji wa miundombinu mijini na vijijini.
Utekelezaji wa zoezi hili unafanyika na kamati inayoundwa na wataalamu kulingana na Mwongozo wa Anwani za makazi wa mwaka 2016.
Wajumbe waliafiki na kushauri kuwa Mpango kazi uandaliwe mapema na uteuzi wa wajumbe ufanyike na lijadiliwe kwenye vikao vya kisheria.

**MUHT.CMT. NA. 14/04/10/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA HATI ZA USAJILI WA VIJIJI 102**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa wakati Halmashauri ya Wilaya inaanzishwa mwaka 2013, ilikuwa na jumla ya vijiji 102. Kati ya Vijiji hivyo baadhi vilikuwa ni vijiji vya zamani vilivyotengwa kutoka Wilaya ya Bariadi na baadhi ya vijiji vilikuwa ni vijiji vipya. Kati ya vijiji hivyo baadhi vilikuwa na hati za usajili na vijiji vipya havikuwa na Hati za Usajili.

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) imesajili upyta vijiji vyote 102 na hati zimepokelewa. Hivyo Hati hizo zitagawiwa kwa vijiji husika kupitia Maafisa Watendaji wa Kata.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuipongeza Serikali kwa usajili huo kwani vijiji vyote vimetambulika kisheria.

**MUHT.CMT. NA. 15/04/10/2021: TAARIFA YA TATHIMINI YA UJENZI WA UZIO WA MINADA YA LAINI NA MIGATO**

Ilielezwa kuwa Kutokana na ulinganifu wa timu ya utafiti inapendekeza kuwa Halmashauri itumie uzio wa msingi wa zege, nguzo za miti iliyowekwa dawa na linked wire.



Scanned with CamScanner

Gharama ya uzio huu ni Tshs. 5,729,300.00 kwa mnada wa Laini na Tshs. 6,267,900.00 kwa mnada wa Migato. Gharama hizi ni ndogo sana ikilinganishwa na kujenga uzio wa msingi wa zege, nguzo za miti iliyowekwa dawa na fence wire.

Wajumbe baada ya majadiliano walishauri gharama zirekebishwe ni kubwa.

**MUHT.CMT. NA. 16/04/10/2021: TAARIFA YA KUTENGEWA FEDHA ZA KUJENGA MAJOSHO MAWILI YA KUOGESHA MIFUGO KIASI CHA TSH.36,000,000.00**

Halmashauri imepokea barua Kumb. Na: CB.173/344/01"L"/12 ya tarehe 9/9/2021 Kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Simiyu ikieleza kuwa katika mwaka wa Fedha 2021/ 2022 Serikali imetenga Tshs.36,000,000.00 (Milioni thelathini na sita tu) kwa wilaya ya Itilima kwa ajili ya ujenzi wa majosho mawili katika vijiji vya wafugaji.

Aidha Halmashauri imetakiwa izingatie vigezo vifuatavyo katika kubaini vijiji/eneo ambapo majosho hayo yatajengwa: Kuwepo na chanzo cha maji cha kudumu, Iwepo ardhi ya kijiji isiyo na mgogoro wowote (kama mwananchi atatoa ardhi yake kuwepo na mhitasari wa kijiji unaobainisha umiliki wa eneo hilo), Liwepo eneo wazi lenye ukubwa wa angalau hekta 1, wananchi wa vijiji husika waukubali mradi na wawe tayari kuchangia nguvu kazi na Josho lizungukwe (kipenyo cha kilomita kumi) na vijiji vyenye idadi ya ng'ombe wasiopungua 4,000. Josho litajengwa kwa utaratibu wa Force Account.

. Halmashauri imetakiwa kufunga mikataba na wazabuni wa vifaa na mafundi wajenzi na kuwasilisha nyaraka za manunuzi kwa Katibu Mkuu Mifugo ili fedha zitolewe. Pia Halmashauri imetakiwa kuhamasisha wananchi ili wachangie nguvu kazi katika kukamilisha miradi hiyo.
Wajumbe waliipongeza Serikali kwa kuweza kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa majosho ya mifugo.

**MUHT.CMT. NA. 17/04/10/2021: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO – 19 TSH.2,450,000,000.00**

Ilielezwa Halmashauri ya wilaya ya Itilima imepokea kiasi cha Sh.2,450,000,000,/= kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika sekta ya elimu na afya. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi wa vyumba vya madarasa 78 katika shule za sekondari- Sh.1,560,000,000/=
ii. Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa shule shikizi- Sh.80,000,000/=
iii. Ununuzi wa mashine za x-ray – Sh.420,000,000/=
iv. Ujenzi wa jengo la huduma dharura hospitali ya Wilaya- Sh.300,000,000/=
v. Ujenzi wa nyumba za watumishi wa sekta ya afya- Sh.90,000,000/=

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuipongeza Serikali kwa juhudi hizo.

**MUHT.CMT. NA. 18/04/10/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI KIIDARA JULAI-SEPTEMBA, 2021**

**UTAWALA NA UTUMISHI**



Scanned with CamScanner

Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizotekelezwa kipindi cha Julai – Septemba, 2021. Shughuli hizo ni pamoja na kupokea watumishi waliohamia kutoka Halmashauri zingine na kuidhinisha uhamisho wa watumishi waliohamia maeneo mengine. Vilevile idara iliweza kushughulikia masuala ya kinidhamu kwa watumishi 4 na hatua zilizochukuliwa.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa. Katika majadiliano, wajumbe waliunga mkono kuwa ni taarifa sahihi.

**IDARA YA ELIMU MSINGI**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizotekelezwa zikiwepo za kubaini maeneo yatakayo stahili kuanzishwa vituo vya ufundi, kufuatilia na kuhamasisha walimu kujiunga na elimu ya watu wazima, kufuatilia ufundishaji wa wanafunzi wa MEMKWA, Kufanya upimaji wa kiwango cha maambukizi ya vimelea vya malaria, kuhamasisha shughuli za uzafi wa mazingira, kufanya ufuatiliaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum na kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji katika shule za msingi.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili. Katika majadiliano, kikao kilisisitiza kusimamia ujenzi wa madarasa kwa fedha zilizotolewa na Serikali.

**IDARA YA ELIMU SEKONDARI**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha shughuli zilizotekelezwa zikiwepo za kusimamia malipo ya walimuwalioenda likizo ya mwezi wa 6/2021, kupokea walimu wa ajira mpya wapatao 45, kuhamasisha na kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa na vyoo kupitia program ya EP4R na COVID – 19 katika maeneo mbalimbali, kusimamia na kuratibu semina mbalimbali kwa walimu wa masomo ya Sayansi.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili. Katika majadiliano, ilibainika kuwa fedha za ujenzi wa madarasa Ikungulipu na Idoselo zilikuwa hazijapokelewa mashuleni. Kikao kilimtaka Afisa Elimu Sekondari afuatilie.

**IDARA YA AFYA**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha Julai – Septemba, 2021, Idara imeweza kufanya safari 37 za usimamizi elekezi katika vituo vya Afya na Zahanati. Pia idara ilifanikiwa kufanya matengenezo ya magari kwa ajili ya kusaidia utoaji huduma mbalimbali kwa jamii.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili. Katika majadiliano, kikao kilipongeza utekelezaji huo.

**IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Idara imeweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi 6 vya wanawake , vijana na watu wenye ulemavu na kuwezesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kupata mikopo ambapo utekelezaji umefanyika jumla ya vikundi 6 vimepata mikopo yenye jumla ya Tsh.38,529,600.00.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuunga mkono kuwa ni taarifa sahihi.

**IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa Idara imeweza kuhamasisha usafi wa mazingira ngazi ya kayana maeneo ya biashara katika vijiji 102, kuhamasisha uhifadhi wa mifuko ya



Scanned with CamScanner

ikolojia ikiwa ni pamoja na upandaji wa miti kwenye taasisi za umma na binafsi na kuhamasisha wananchi matumizi ya njia za kukabiliana na magonjwa yanayosababishwa na hali mbaya ya usafi na mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi kama vile COVID-19, Malaria, kuharisha nk.
Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuijadili. Katika majadiliano wajumbe walihoji kutaka kufahamishwa usimamizi wa eneo la kutupia taka ngumu. Wajumbe walimtaka Afisa Usafi na Mazingira awasiliane na Afisa Ardhi ili waende kuhakiki eneo hilo na kuliewekea alama. Vilvile kuhusu usafi wa mazingira, ufanyike ufuatiliaji wa ada za Usafi wa Mazingira kwa kushirikiana na Afisa Mapato.

**IDARA YA KILIMO**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha Julai – Septemba, 2021, Idara imeweza kufanya Usimamizi wa uvunaji wa zao la pamba,ubora wa pamba na uuzaji kwa wakulima msimu wa kilimo 2020/2021 kupitia vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS)., Usimamizi wa ununuzi wa pamba kupitia makampuni ya ununuzi wa pamba, Kuendesha mafunzo maalumu kwa wakulima kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba kwenye zao la Pamba, Usimamizi wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia nafaka katika Kijiji cha Ikindilo, Kuandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara ya kilimo, umwagiliaji na ushirika na Utatuzi wa migogoro kwenye vyama vvya msingi.
Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuijadili. Katika majadiliano kikao kilishauri Afisa Kilimo awasilishe mpango mzuri wa ukusanyaji wa ushuru wa mazao mchanganyiko na awasilishe orodha ya makapuni yaliyonunua pamba ambayo bado yanadaiwa ushuru.

**IDARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha robo ya I 2021/2022, Idara imeendele kusimamamia Wafugaji kufanya shughuli za uogeshaji mifugo yao kwa Kutumia majosho yaliyopo kuogesha mifugo ili kuthibiti magonjwa yaenezwayo na kupe. Wafugaji wa kijiji cha Bumera, Sawida, Nhobola, Mwamtani, Mwalushu na Lugulu wanaendelea kuogesha mifugo.
Pia Wafugaji wameshauriwa Kutoingiza mifugo kwenye hifadhi ya wanyama pori ili kuepuka magonjwa yatokayo kwa wanyama pori kwenda kwa wanyama wafugwao. Ushauri huu umetolewa kwa wafugaji wa vijiji vya kata ya Mwamtani Nkuyu, Mwaswale na Migato.
Vilevile Idara imeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wafugaji, kwa kutembelea mifugo yao na kutoa tiba kwa magonjwa mbalimbali yaliyojitokeza. Pia kutoa ushauri juu ya utunzaji wa malisho ya mifugo na unyweshaji wa dawa za minyoo ii kupata tija zaidi kutokana na mifugo. Ilielezwa kuwa katika robo hii Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mh. Mashimba Mashauri Ndaki (MB) alifanya ziara Wilayani Itilima katika kijiji cha Longalombogo na kuzindua zoezi la utambuzi wa mifugo kwa njia ya hereni. Pia Idara inaendelea kutekeleza Miradi ya ujenzi wa Majosho mawili ya Ngeme na Mwandulu kwa ufadhili wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ,Halmashauri ya Wilaya ya Itilima na Wananchi wa Vijiji hivyo.
Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa. Katika majadilano, wajumbe walishauri Afisa Mifugo na Uvuvi afuatilie takwimu za mifugo zinazowasilishwa kwenye kikao kwani zinaonekana kufanana na taarifa ya vikao vilivyopita.



Scanned with CamScanner

**IDARA YA UJENZI**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha Julai – Septemba, 2021, Idara imeweza kufanya Usimamizi wa Ujenziwa jengo la utawala awamu ya tatu. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa stoo ambao uko hatua ya kuta za boma, ujenzi wa maegesho ya magari uko hatua ya umaliziaji na ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji, kuhifadhi na kusambaza maji kwenye jengo ujenzi wa mnara wa tanki umekamilika na ujenzi wa tanki uko hatua ya umwagaji wa zege la kufunika tanki. Ilielezwa pia kuwa Vilevile Ujenzi wa jengo la utawala awamu ya nne unaendele kutekelezwa ambapo Mradi huu unahusisha ujenzi wa uzio, karakana, nyumba ya mlinzi, canteen, power house, landscaping na uwekaji wa paving block. Mradi huu uko katika hatua za awali.

Aidha ilielezwa pia kuwa Ujenzi wa wodi tatu ( wodi ya watoto, wanaume na wanawake) katika Hospitali ya Wilaya ambapo Wodi ya wanaume ujenzi uko hatua ya ufungaji wa mfumo wa maji safi na maji taka, wodi ya wanawake ujenzi uko hatua ya upigaji wa lipuna wodi ya watoto ujenzi uko hatua ya skimming pamoja na upachikaji wa vigae.

Ilielezwa kuwa hali ya hewa, utekelezaji ulianza kipindi cha mvua ilipelekea magari yaliyokuwa yanapeleka vifaa kama saruji, mchanga, kokoto, moramu kukwama kabla ya kufika eneo la kazi, Ukamilishaji wa zahanati tatu( zahanati ya Laini, Dasina na Nhobora) ambao uko hatua ya uwekaji wa sakafu kwa ajili ya kupokea vigae kwa zahanati ya Nhobora,uwekaji wa sakafu katika zahanati ya Laini na Dasina na mfumo wa maji safi na taka katika zahanati zote na Ujenzi wa kituo cha afya Kanadi– ujenzi uko katika hatua za awali

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa. Baada ya majadiliano wajumbe waliunga mkono kuwa taarifa ni sahihi.

**IDARA YA MALIASILI**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha Julai – Septemba, 2021, Idara imeendelea kutoa elimu kwa wanachi na vikundi binafsi kwa kushirikiana na Wakala wa huduma za misitu Tanzania kwenye vijiji vya shishani, Mwaswale, Mwamtani, Nkuyu, Nyantugutu, Isengwa na Ngesha. Mwamapalala, Lagangabilili,Mwanunui, Idosero, Migato, isengwa na Ngwalali, Pijuru, Longolambogo,

Vilevile Miradi miwili ya vitalu vya miti imeanzishwa katika shule ya secondary Lagangabilili na shule ya msingi ikungulipu A kwa kushirikiana na wakala wa huduma za Misitu Tanzania. Kuhusu Doria ilielezwa kuwa jumla ya doria 20 zimefanyika katika mapito makuu ya wavunaji haramu wa mazao yatokanayo na misitu.

Ilielezwa kuwa tathmini zimeendelea kufanyika katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Itilima kwa kushirikiana na Idara ya Mifugo, Kilimo na Afya, Mamlaka ya usimamizi wa Wanyamapori (TAWA). Jumla ya doria 22 za ndani ya Wilaya zimefanyika na kufanikiwa kuwadhibiti Wanyamapori waharibifu. Jumla ya makundi 18 ya Tembo yalidhibitiwa. Jumla ya watuhumiwa wanne (4) walikamatwa kwa makosa mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuingia hifadhini bila kibali na kosa la kumiliki nyara zitokanazo na Wanyamapori bila kibali.



Scanned with CamScanner

Jumla ya ekari 4718.5 zinatumika kwa shughuli za kibinadamu ndani ya Bufferzone, shughuli kuu zikiwa ni kilimo na ufugaji. Jumla ya watu 2860 wanaishi ndani ya maeneo ya Bufferzone.

Taarifa ilipokelewa na kujadiliwa. Katika majadilano kikao kilishauri Afisa Maliasili afuatilie ukataji holela wa miti unaojitokeza katika maeneo mabalimbali kwenye vijiji na kwenye bwawa la Mwalushu.

Aidha kuhusu kuhusu barabara ya kwenda Sopa Lodge, kikao kilimtaka Afisa Maliasili afanye ufuatiliaji wa kujua hatua iliyofikiwa kuhusu ufunguzi wa barabara ya kwenda Sopa Lodge kutoka Mwaswale kupitia Maswa Game Reserve.

**KITENGO CHA SHERIA**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha Robo ya kwanza 2021/2022 kitengo kimeweza kushughulikia Kesi ya madai dhidi ya wavamizi wa eneo la machinjio ambapo Bwana Kacheli Sulwa, Dida Biliya na Maige Shenye wamejimilikisha eneo hilo lenye ukubwa takribani robo tatu ya ekari.

Kuhusu Kesi ya KACHELI SULWA & 2 OTHERS ***VS***IDOSELO VILLAGE COUNCIL. Ilielezwa kuwa kesi hii awali ilikuwa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ikihusisha madai dhidi ya wavamizi wa eneo la machinjio ambapo bwana Kicheli Sulwa, baada ya hukumu ya Baraza kuipa ushindi Halmashauri ameamua kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo Mahakama Kuu Kanda ya Shinyanga. Ilipangwa kusikilizwa tarehe 22/10/2021.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuijadili. Baada ya majadiliano waliunga mkono kuwa taarifa ni sahihi.

**KITENGO TEHAMA**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa , kitenge kimeweza Kuendeleza na kusimika mfumo wa Mfuko wa afya ya jamii iliyoboreshwa (iCHF) kwenye simu za Maafisa Waandikishaji wapya ili waweze kuandikisha wanachama wapya wa iCHF, Kuendeleza zoezi la kusimika mfumo wa madai wa CHF iliyoboreshwa kwenye simu za watumishi wa Zahanati na vituo vya afya vilivyopo Halmashauri ya wilaya ya Itilima ili waweze kudai madai yao pindi wanachama wa CHF iliyoboresha wanapotibiwa katika vituo vyao, ufungaji wa mtandao Kiambo (LAN) katika wodi tatu (3) za watoto, wanawake na wanaume zilizopo Hospital ya wilaya, kituo vya Afya kanadi na zahanati zote zisizo kuwa na miundo mbinu mtandao kiambo (LAN) na zinatumia Mfumo wa GOT-HOMIS, kufanya marekebisho ya miundo mbinu ya mtandao kiambo (LAN) katika Jengo la Mkurugenzi mtendaji na mifumo ya yote ya TAMISEMI imekamilka na inatumika vema. pia kufanya marekebisho ya miundo mbinu ya mtandao kiambo (LAN) katika Hospitali ya wilaya (Nguno), vituo vya Afya na zahanati.

Vilevile kazi zilizofanyika ni pamoja na Kununua vifaa kwa ajili ya kutimiza majukumu ya maafisa Tehama kama Printa ya kutolea vitambulisho, Kuendelea kuishauri Halmashauri juu ya matumizi sahihi ya mifumo na namana ya kuendesha kituo cha mawasiliano (TELECENTER)kwa faida zaidi bila madeni toka Halmashauri yenyewe, Kuendelea Kutoa ushauri kwa kila idara na vitengo juu ya ununuzi wa program za ulinzi(Ant virus) pamoja na kusimika program hizo kwa ajili ya ulinzi wa kompyuta za Halmashauri na Kufanya matengenezo madogo madogo ya kila siku ya kompyuta za Halmashauri.



Scanned with CamScanner

**KITENGO CHA UCHAGUZI**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika robo ya kwanza kazi iliyofanyika ni kuhakiki maeneo ya utawala na ufuatiliaji wa maeneo ya Vijiji na Vitongoji ambayo yapo wazi kutokana na viongozi wa maeneo hayo. Ilielezwa kuwa kuna nafasi wazi 14 za wenyeviti wa Vitongoji na nafasi wazi 34 za wajumbe wa Serikali za Vijiji ambapo nafasi hizo zimetokana na baadhi kujiudhuru, kustaafishwa uanachama na wengine kufariki.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuunga mkono kuwa taarifa ni sahihi.

**KITENGO NYUKI**

Taarifa iliwasilishwa kwa kuelezwa kuwa katika kipindi cha robo iliyopita, kitengo kimefanya Ukaguzi wa manzuki za vikundi vya ufugaji nyuki pamoja na ukusanyaji wa taarifa na takwimu za ufugaji nyuki wilaya, Utoaji mafunzo kwa vikundi vya ufugaji Nyuki juu ya ubora wa mazao ya Nyuki na uhamasishaji kwa wafugaji wapya, Kuondoa na kuhamisha makundi ya nyuki kwenye makazi ya watu. Vilevile kutoa elimu na kutembelea maeneo mapya ya uanzishwaji wa manzuki, wananchi watano (5) na vikundi vitatu wamefikiwa na kupewa elimu na kuwatafutia wafugaji wa nyuki masoko ya asali na nta ndani nan je na wilaya.

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kuijadili. Baada ya majadiliano waliunga mkono kuwa taarifa ni sahihi.

**MUHT.CMT. NA. 19/04/10/2021: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA KMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO TAREHE 17/09/2021**

Utekelezaji wa maazimio ya kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha tarehe 17/09/2021 uliwasilishwa. Wajumbe waliwataka wahusika kwenye maazimio hayo wahakikishe wameyajibu kwa ufasaha.

**MUHT.CMT. NA. 20/04/10/2021: KUAHIRISHA KIKAO.**

Katibu alimkaribisha mwenyekiti, Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa kuwa na ushirikiano wakati wote wa kikao akaahirisha kikao mnamo saa 08:40 Mchana na kuwatakia wajumbe majukumu mema..

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

Leo tarehe 12/11/2021
Saini [signature]
Jina Michael Tolape
**KATIBU**

Leo Tarehe 12/11/021
Saini [signature]
Jina ELIZABETH M Gunso
**MWENYEKITI**



Scanned with CamScanner